

TUNAKUTUKUZA

♩=70

Munywoki Martin Mutua
04.04.2020
Kakumuti, Kitui

VERSE

1.Pa nde zo te za du ni a, Vi u mbe wa ko wo te waku sha ngi
U me ku wa mwa mi ni fu, Wa tu ku mbu ka si si tu li o dha

5 li a, Wa tu wa na ku i nu a, na si tu na ku i mbi a.
i fu, Tu so ju a ku ku si fu, we we mwe nye u tu ku fu.

9 BRIDGE

Tu na ku tu ku za - - - Tu na ku tu

1.Kwa ze ze na vi na nda, ba ra gu mu na pa - nda,

Tu na ku tu ku za Tu na ku tu

13

ku za - - Tu na ku tu ku za - - Tu na ku tu

Nde re mo zi me ta nda Na ngo ma zi na du - nda

ku za Tu na ku tu ku za Tu na ku tu

CHORUS

i ye ee a i ye ee a i ye

17

ku za a e ho ye ho ye a e ho ye ho ye a e

ku za

ee A i ye

22

ho ye tu na ku tu ku za a e tu na ku tu ku za

TUNAKUTUKUZA

3

@Martin Munywoki

1. Pande zote za dunia, viumbwe wako wote wakushangilia,
Watu wanakuinua, nasi tunakuimbia;
Umekuwa mwaminifu, watukumbuka sisi tulio dhaifu,
Tusojua kukusifu, wewe mwenye utukufu.

*Kwa zeze na vinanda - tunakutukuza
Baragumu na panda - tunakutukuza
Nderemo zimetanda - tunakutukuza
Na ngoma zinadunda - tunakutukuza*

*Iyee (ae hoye), aiyee (ae hoye) aiyee (ae hoye) tunakutukuza
Aiye (ae hoye), aiyee (ae hoye) aiyee (ae hoye) tunakutukuza*

2. Sina budi kushukuru, ulinivua giza kanivika nuru,
Utumwa kaninusuru, kaniweka niwe huru;
Japo mimi hukosea, hujanitupa bado wanihurumia,
Hata ninapopotea, wanielekeza njia.

*Kwa nyimbo na zaburi - tunakutukuza
Filimbi na zumari - tunakutukuza
Kayamba na matari - tunakutukuza
Na kwa sauti nzuri - tunakutukuza*

3. Unipaye bure hewa, kunitetea kila ninapoonewa,
Kwako sijapungukiwa, wala sijaelemewa;
Unayenipa mkate, na kunilinda kote wakati wowote,
Nijalie nisisite, kukusifu siku zote.

*Sifa zote ni zako - tunakutukuza
Huko juu uliko - tunakutukuza
Vigelegele, heko - tunakutukuza
Na shangwe na chereko - tunakutukuza*

* * *

*Una neema tele - tunakutukuza
Tangu enzi za kale - tunakutukuza
Na umebaki vile - tunakutukuza
Milele na milele - tunakutukuza*

*Wasio na chakula - unawapokea
Wasona pa kulala - unawapokea
Wajapo kwako bila - unawapokea
Unawajibu sala - unawapokea*

* * *

*Vipofu wanaona - wanakutukuza
Viwete wanapona - wanakutukuza
Tasa wapata mwana - wanakutukuza
Na bubu wananaena - wanakutukuza*

*Kweli wewe ni baba - tunakutukuza
Daima watubeba - tunakutukuza
Kwako twapata tiba - tunakutukuza
Watukinga misiba - tunakutukuza*